

**Umishenari wa Kupanda
Makanisa Mashinani
mwa Miji Mikuu**

SLP 7 * Grandville, Michigan 49468
UNITED STATES OF AMERICA
Barua Pepe: danielschutte@sbcglobal.net
www.citiesforchrist.org

(616) 970-4432

*BWANA YESU KRISTO na
Neno LAKE Mashinani mwa miji Mikuu*

**“MUNGU
ANAKUPENDA
WEWE”**

MUNGU ANAKUPENDA WEWE

Je, wewe unajua kwamba MUNGU anakupenda? Ndiyo, anakupenda sana! YEYE anakupenda sana. YEYE anakupenda sana, mpaka akamtuma mwana wake wa pekee, YESU KRISTO, ili afe kwa ajili yako. Biblia Kitabu cha Mungu, kinatuambia hivi “Kwa maana jinsi hii, MUNGU aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwana wake wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.” Yohana 3:16

Je, wewe unashangaa ni kwa nini ilimbidi YESU KRISTO afe kwa ajili yako? Naam Biblia inasema hivi “....Hakuna mtu atendaye mema, hakuna hata mmoja. Kwa sababu wote wametenda dhambi, wakupungukiwa na utukufu wa MUNGU” Warumi 3:12 b, 23.

Hii inamaanisha ya kwamba kila mtu ulimwenguni ametenda mambo fulani mabaya maishani mwake, kama tu wewe na Mimi. Kwa mfano, ukimkasirikia Dada au Kaka wako, ama mtu mwingine fulani shuleni bure. Ama usipotii wazazi wako na kutenda vile wanataka ufanye. Wala unapodanganya na kukosa kumwambia mtu fulani ukweli.

Hiyo ndiyo sababu ilimbidi Yesu afe. Alikufa kwa mahali petu, kwa ajili ya mambo mabaya tuliyoyatenda. Mungu hapendi tukitenda dhambi. Inamuumiza na kumhuzunisha sana. Lakini kuna kitu kimoja tu ambacho kinaweza kumfanya Mungu asamehe na kusahau maovu yetu. Je, unadhani hicho kitu ni nini? Naam, sio kwenda Kanisani au shule ya Jumapili. Wala sio kwa sababu wazazi wetu huenda kanisani. Hicho kitu kimoja, sio sababu eti sisi ni watu wazuri. MUNGU anaweza tu kusamehe na kusahau maovu yako, na kukupeleka mbinguni siku moja, mradi tu, ukiamini ya kwamba, MWANA wake YESU KRISTO alikufa kwa sababu ya dhambi zako. Angalia katika Yohana 03:18 tena “Kwa maana jinsi hii MUNGU aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwana wake wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.” Inasema ya kwamba ukimwamini Mwana wa MUNGU, YESU KRISTO, hautaangamia (ama kwenda Jehenamu) bali utapata uzima wa milele. Na hii inamaanisha ya kwamba utaishi na YESU mbinguni milele.

Je, utamwamini yeye leo?